# TNMC Habari

Toleo No. 0015

TOLEO MAALUMU

Novemba, 2024

HALIUZWI

www.tnmc.go.tz @tnmchabari


# Tanzania Kuendeleza Vita Dhidi Ya Malaria, Kifua Kikuu , Virusi Vya Ukimwi




Habari Uk. 01

**"Tunajua kama vita kamili dhidi ya Magonjwa ya Maleria, Kifua Kikuu na UKIMWI yanahitaji mifumo ya Afya iwe vizuri, "**

## DC Mapunda Afunga Chuo Cha Uuguzi, Ukunga Temeke na Aagiza Mkurugenzi Wake Akamatwe

Habari Uk. 06











Jarida Maalumu
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlakaya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI

## MWENYEKITI

**Bi. Agnes Mtawa**

## MHARIRI

**Mwakapiso Ndimmyake**

## WARATIBU

**Irene Chilewa**
**Rose Mhando**

## MSANIFU JARIDA

**Ezekiel Nyalusi**

P.O BOX1736 DODOMA

# Tanzania Kuendeleza Vita Dhidi Ya Malaria, Kifua Kikuu Na Virusi Vya Ukimwi



Na. Mwandishi wetu

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu, amesema Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na mataifa mengine duniani kupitia Mfuko wa Dunia (Global Fund) inaendelea kuongeza, kuunganisha jitihada na nguvu kuhakikisha wanatomeza Malaria, Kifua Kikuu na virusi vya UKIMWI Duniani.

Dkt. Jingu amesema hayo Novemba 22, 2024 jijini Lilongwe nchini Malawi, wakati akishiriki kikao cha 52 cha Bodi ya Mfuko wa Dunia (52nd Global Fund Board) ambacho kimejadili hatua za kuimarisha mapambano dhidi ya magonjwa ya Kifua Kikuu, Malaria na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Dkt. Jingu amesema kufuatia dhima ya mkutano huo kama nchi wameona namna nzuri ni kushirkiana na nchi zingine kupitia Mfuko wa Dunia.

*"Ni kazi ambayo ni kubwa lakini kwa kiwango kikubwa ni kwamba tunaunganisha pamoja jitihada na nguvu za Dunia kuhakikisha maadui hawa wakubwa watatu tunawatokomezwa kabisa," alisema, Dkt. Jingu*

Dkt Jingu, ameongeza kuwa ili kufanikisha vita dhidi ya magonjwa hayo, mifumo bora na madhubuti ya Afya inahitajika na mfuko wa Dunia (Global Fund) kushirikiana na Serikali

> *"Tunajua kama vita kamili dhidi ya magonjwa ya Maleria, Kifua Kikuu na UKIMWI yanahitaji mifumo ya Afya iwe vizuri, "*

Serikali imekuwa ukisaidia Tanzania kuimarisha mifumo ya Afya.

"*Mojawapo ya kazi za mfuko wa Dunia ni kuimarisha mifumo ya Afya, tunajua kama vita kamili dhidi ya magonjwa ya Maleria, Kifua Kikuu na UKIMWI yanahitaji mifumo ya Afya iwe vizuri, Sisi kama nchi (Tanzania) tunanufaika sana na rasilimali ambazo tunazipata kutoka kwenye Mfuko wa Dunia na kuchochea nguvu ya mapambano kwa kiasi kikubwa katika vita yetu dhidi ya magonjwa haya matatu,*" amesema Dkt. Jingu.

Kikao hicho ambacho kimehitimishwa Novemba 22, 2024 pia kilijadili mchango wa Mfuko wa Dunia kwenye masuala ya haki za binadamu na usawa wa kijinsia, mabadiliko ya tabia nchi na Afya, uwekezaji, uendelevu na sera ya ufadhili wa pamoja.

Bodi ya Mfuko wa Kimataifa hukutana mara mbili kwa mwaka na Dkt. Jingu anashiriki kikao hicho kama Mjumbe wa Bodi hiyo akiwakilisha nchi za Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika (Eastern and Southern Africa - ESA).

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

# SALAMU ZA POLE

Dkt. Faustine Ndugulile



## 1969 - 2024

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania tumepokea kwa Masikitiko taarifa ya kifo cha Dkt. Faustine Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni pia Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kanda ya Afrika. Tunaungana na Familia, na Watanzania wote katika kuomboleza Msiba huu.

***BWANA AMETOA, BWANA AMETWAA,***
***PUMZIKA KWA AMANI.***

@tnmchabari www.tnmc.go.tz

# Bima Ya Afya Kwa Wote Kudhibiti Ongezeko La Magonjwa.

**Na. Mwandishi wetu**




Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Afya, Bw. Amoury Amoury, amesema mpango wa Serikali wa kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote utasaidia kudhibiti ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza na kuwezesha wananchi kumudu gharama za matibabu.

Bw. Amoury amebainisha hayo Novemba 14, 2024 Jijini Dodoma katika wiki ya magonjwa yasiyoambukiza katika kikao kazi cha kujadili mikakati ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza nchini, ambacho kimehusisha Wizara 15 za kisekta pamoja na wadau mbalimbali.

Bw. Amoury amesema kuwa, bima ya Afya itawasaidia wananchi kudhibiti ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza na kila mwananchi atapata huduma za uchunguzi pamoja na matibabu pale atakapozihitaji bila kikwazo cha fedha.

***“Sheria hii ya bima ya Afya kwa wote pia itamkinga mwananchi kulipia huduma ambazo zinaweza kumsababishia umaskini ambapo tumeshudia baadhi ya wananchi wasio na bima ya Afya wakiuza mali ili waweze kugharamia matibabu,”*** amesema Bw. Amoury.

“Wananchi walio na bima ya *Afya hadi sasa ni asilimia 15, asilimia 85 ya wananchi hugharamia matibabu kwa malipo ya papo kwa papo,”* amebainisha Bw. Amoury.

Aidha, ameeleza Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote inaweka ulazima kwa kila mwananchi kuwa na bima ya Afya ambayo itawezesha kila mwanachi kutibiwa na kuondoa dhana na mazoea yaliyopo ambapo mgonjwa huenda hospitali pale anapokuwa katika hali mbaya.

***“Kwa kuwa na bima ya Afya mwanachi ataenda hospitali mapema kabla ya kuwa na tatizo kubwa la ugonjwa na hivyo kutibiwa mapema na kuokoa gharama kubwa ambazo zingetumika kutibu ugonjwa ukiwa katika hali mbaya,”*** ameongeza Bw. Amoury.



# Katika Ajali ya Kuanguka kwa Jengo Kariakoo Dkt. Mollel Aipongeza Timu ya Uokoaji katika




**Na. Mwandishi Wetu.**

Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, ametoa pongezi hizo kwa timu ya uokoaji katika ajali ya kuanguka jengo la kariakoo baada ya kufika kujionea hali halisi katika ajili hiyo.

***"Kazi inayoendelea hapa imefanywa kwa umakini wa hali ya juu na Jeshi letu na timu ya uokoaji, kuhakikisha watu walioko ndani ya vyumba vya majengo jirani hawafunikwi na vifusi.***

***Mimi binafsi nimeingia katika baadhi ya vyumba vya majengo ya jirani ambayo yamekuwa njia ya kuingia kwenye jengo lililoanguka," amesema Dkt. Mollel.***

Aidha, Ameongeza kuwa umahiri na uangalifu wa vikosi vya uokoaji umewezesha majeruhi wengi kufikishwa hospitalini wakiwa na majeraha madogo au bila majeraha makubwa, na hali zao zinaendelea kuimarika.

Hata, hivyo kwa mujibu wa Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba, amesema miili mitatu kati ya miili ya Watu 29 ambao wamefariki, bado haijatambuliwa lakini miili 26 imetambuliwa na tayari imechukuliwa na Ndugu zao kwa ajii ya maziko huku akisema zoezi la uokoaji limehitimishwa na biashara zitaruhusiwa kuendelea kama kawaida.





# Kelekea Mtihani Wa Usajili Na Leseni Watahiniwa Waaswa Kuzingatia Taratibu Za Maombi Ya Mtihani.

Na. Ezekiel Nyalusi



Akizungumza na TNMC Habari Kaimu Mkurugenzi wa kurugenzi ya Maendeleo ya taaluma Bw. John Kafumu amewataka watahiniwa watarajiwa kuzingatia taratibu zote za maombi ya mtihani wa usajili na leseni.

***"Ni muhimu kwa muombaji wa Mtihani huu wa usajili na leseni kuhakikisha anakuwa na vigezo vyote kabla ya kuanza kuomba: moja Kuwa na namba ya utambulisho (Indexing Number), kwa mujibu wa kifungu cha 14 (1) cha kanuni za mafunzo, Pili awe amefaulu mtihani wa kufuzu mafunzo kwa ngazi husika (qualifying examination),"*** alisema Kafumu

Katika hatua nyingine Bwana kafumu Amebainisha kuwa kuwa dirisha la maombi limefunguliwa tangu tarehe 04.12.2024 na Maombi yatafanyika mtandaoni kwa kutumia mfumo wa Baraza ***www.tnmc.tnmcis.go.tz.*** ambapo, mwombaji kwa mara ya kwanza atatakiwa kujisajili na kulipia kiasi cha Shilingi 150,000/= na kwa wanaorudia watalipia kiasi cha Shilingi 75,000/=

Aidha, kafumu akasisitiza pia suala la mtahiniwa kuhakikisaha ana weka picha sahihi ***(Passport Size 45mmX35mm),*** Kujaza majina sahihi yanayoendana na vyeti vya kumaliza elimu ya sekondari, Kufanya malipo na kuchagua kituo sahihi cha mtihani kwa wakati.









# DC Mapunda Afunga Chuo Cha Uuguzi, Ukunga Temeke, Aagiza Mkurugenzi Wake Akamatwe



*"Nikiwa kama Mkuu wa Wilaya ya Temeke, kuanzia leo natangaza kukifunga chuo hiki kwa kukiuka maelekezo ya Serikali, ambapo kuanzia leo Wanafunzi wote hawa warejee makwao hadi pale uongozi wa chuo hiki utakaporekebisha Kasoro zilizopo, pia naagiza kukamatwa kwa Mkurugenzi wa Chuo hiki aje atueleze **kwanini amekiuka** Maelekezo ya Serikali"* amesema DC Mapunda.

Hata hivyo, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania linawataka wazazi na walezi kuhakikisha wanafuatilia usajili wa vyuo vya kada za Uuguzi na Ukunga kabla ya kuwapeleka Watoto wao huku likiwataka watu binafsi kufungua vyuo kwa kufuata tarajibu na miongozo ya kitaaluma hiyo.

**Na. Mwandishi wetu**

Mkuu wa Wilaya ya Temeke Sixtus Mapunda amekifungia Chuo cha Kewovac kinachojihusisha na utoaji wa Elimu ya Uuguzi na Ukunga kilichopo Mbagala Charambe kwa kutokidhi vigezo vya utoaji Elimu hiyo na ubovu wa mazingira kwenye Chuo hicho.

Sambamba na kutangaza kukifungia, DC Mapunda pia ameagiza kukamatwa kwa Mkurugenzi wa Chuo hicho na wasaidizi wake ili kwenda kujibu tuhuma zinazowakabili ikiwemo kukiuka agizo la Serikali la kukifungia Chuo hadi pale kitakapoweka mazingira rafiki kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma hapo.

Akitangaza uamuzi huo Jijini Dar es Salaam baada ya Kufika na kufanya Ukaguzi kwenye Chuo hicho, DC Mapunda amesema Makosa mengine yanayomkabili Mkurugenzi huyo ni Pamoja na kutofuata mtaala wa Serikali unaoagiza elimu ya Uuguzi na Ukunga kufundishwa kwa miaka miwili na si mwaka mmoja kama kinavyofanya chuo hicho.



# Watoa Huduma Chumba Cha Upasuaji Mtwara - SZRH Wanufaika Na Mafunzo Kutoka TNMC.

Na Mwandishi Wetu



Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), limetoa mafunzo elekezi kwa Madaktari, wauguzi,wakunga na wauguzi wataalamu wa dawa za usingizi na ganzi wanaofanya kazi katika vyumba vya upasuaji pamoja na baadhi ya watumishi kutoka vitengo mbalimbali vya kutolea huduma wapatao 45 katika Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini, juu ya namna bora ya kutoa huduma katika chumba cha Upasuaji ***"Theatre Management"*** kwa lengo la kumlinda mgonjwa kuwa salama baada ya upasuaji.

Mafunzo hayo yaliyodumu kwa muda wa siku 14 yameongozwa na Afisa Muuguzi Mbobezi kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Salome Kassanga, akisaidiana na Muuguzi mbobezi katika chumba cha upasuaji Bi Happiness Liya kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Ligula.

***"Tunatoa mafunzo haya ili kuhakikisha kuwa vyumba vya upasuaji kunakuwa na misingi bora ya usimamiaji na uendeshaji, misingi ya kudhibiti maambukizi kwa wagonjwa (IPC), uzingatiaji wa Maadili, Sheria, kanuni na miongozo katika chumba cha upasuaji, kulingana na miongozo husika, uzingatiaji wa kuweka taarifa za wagonjwa wanaopatiwa huduma za upasuaji (Documentation), pamoja na kulinda usalama wa mgonjwa na watoa huduma"*** alisema Bi. Kassanga.

Hata hivyo, Bi. Kassanga ametumia nafasi hiyo kuwakumbusha watumishi juu ya utoaji wa huduma kwa kuzingatia Maadili, Miiko, Uadilifu, ikiwa ni Pamoja na uvaaji wa Sare maalumu za chumba cha upasuaji kulingana na miongozo husika, uzingatiaji wa kuweka taarifa sahihi za wateja wanaopatiwa huduma ***(Documentation)***, pamoja na kulinda usalama wa mgonjwa na watoa huduma" alisema Bi. Kassanga.



# Tanzia

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi Oktoba, 2024, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.



JINA  ASMA MANDA
KITUO: Hospitali ya Temeke
MKOA: DSM



JINA: JESCA KATAMBI
KITUO: Geita RRH
MANISPAA: Geita.
MKOA: Geita



JINA: RODA MITANDA
KITUO: Kituo cha Afya Hanet
WILAYA: Chamwino
MKOA: Dodoma



JINA: BUTERA KIBENGERA
KITUO: Chazi
WILAYA: Mvomelo
MKOA: Morogoro



JINA: HUSSEIN MWAKASALA
KITUO: KCMC
MKOA: Kilimanjalo



JINA: JMKAMA MKENGEJI
KITUO: Hospitali ya Rorya
WILAYA: Rorya
MKOA: Mara

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu: 0736 00 60 60**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA